

Kutathmini Vipengele vya Lugha Vilivyotumiwa katika Michezo ya Kuigiza Kuhusu Ukimwi katika Mashindano ya Sanaa za Shule za Upili.

Michael Kiguta.

Laikipia University, Kenya.

Email: mchkiguta@yahoo.com

IKISIRI

Utafiti huu unalenga kutathmini vipengele vya lugha vinavyotumiwa katika michezo ya kuigiza kuhusu ukimwi katika mashindano ya sanaa za shule za upili. Nadharia iliyotumiwa ilikuwa ya umaumbo. Maeneo ya utafiti yalitokana na uchunguzi wa michezo miwili, ambayo ilikuwa: *Chozi* (2001) na *Majuto* (2001). Tulitumia michezo kama sampuli iliyowakilisha michezo yote ya Kiswahili iliyo'uwa na mada kuhusu ukimwi. Uteuzi ulitokana na sababu kuwa ulihusu vipengele vya kimsingi kama vile: uhusika, mandhari, jukwaa, kitendo, ploti, lugha maleba na jumuiya. Utafiti huu ulikuwa wa kimaktabani ulitumia hadhira tuli ya kimaandishi. Data zilizokusanywa kutoka nakala za michezo ziliainishwa kupitia kigezo cha matumizi ya lugha. Utafiti huu ulibaini kuwa lugha ya kisanii ilitumiwa katika tamthilia za shule za upili. Lugha iligawanywa kwa mifumo ya mbinu za kiishara na viambajengo vya umuundo. Mifumo ya ishara, maana ya lugha ya kiisimu na taashira za lugha zilitumiwa kujenga tamthilia. Tafiti hii inapendekeza tamthilia kujengwa vizuri kwa njia ya kisanaa kwa kutumia lugha yenye mvuto na mnato kusababisha ujumbe uliofaa, vile vile, wasanii wanahitaji kufanya utafiti mkubwa zaidi kuhusu sanaa ya lugha kwa kuwa ndiyo sehemu ya umuundo na unahitaji ufundi mkubwa.

Maneno muhimu: Vipengele vya lugha, michezo ya kuigiza, ukimwi, sanaa za shule za upili.

How to cite this article in APA.

Kiguta, M. (2021). Kutathmini Vipengele vya Lugha Vilivyotumiwa katika Michezo ya Kuigiza Kuhusu Ukimwi katika Mashindano ya Sanaa za Shule za Upili. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 4(1), 368-373. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v4i1.356>

UTANGULIZI

Ukimwi ni miongoni mwa majanga makubwa katika taifa la Kenya. Ni tisho lililo kubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na ukweli kwamba suluhisho bado halijapatikana. Mnamo mwaka wa 1999, Serekali ya Kenya ilitangaza kuwa ukimwi ni janga la taifa. Malengo makuu ya sera ya taifa yalizindua vyombo mbalimbali, miradi na mikakati ya kupambana na maenezi ya ugonjwa huu. Kupitia kigezo cha utafiti huu, tulitathmini nguvu ya fasihi, kama njia mojawapo iliyotumiwa na watunzi kupasha habari kupitia tamasha za maigizo za shule za upili na vyuo. Tamasha hizi zilifanyika mwezi wa Februari hadi mwanzoni mwa Aprili katika kalenda ya shule ya kila mwaka. Tulitumia nakala za tamthilia Choji (2001) na Majuto (2001), kufikia malengo ya mada yetu. Tulitathmini kazi ya wasanii na kuchunguza matumizi yao ya lugha na mbinu za kisanaa pamoja na maudhui yaliyotumiwa kuzijenga kazi zao. Nakala hizo za tamthilia zilitusaidia kukusanyia data ya uhakiki.

Tulichunguza sifa za utendaji na uigizaji kama vile; matumizi ya vitabia, miondoko, ishara za mikono, nyuso, macho, mwili, matumizi ya sauti, kiimbo, kasimawimbi, kidatu na tambo ambazo zilitumiwa katika mawasiliano. Kigezo cha uteuzi wa kilitokana na swala nyeti la ukimwi. Kigezo kingine kilitokana na sababu kuwa michezo hii ndiyo iliyokuwa miongoni wa ile iliyofanya vizuri katika ngazi za kitaifa. Jambo lingine muhimu ni kuwa zilitungwa katika kipindi cha mwisho wa miaka ya themanini, wakati ukimwi ilikuwa umeanza kushika kani na kushamiri. Ingawa tamthilia hizi hazijawahi kuchapishwa, zilitupa malighafi ya kufaa ya kukusanyia data. Hata hivyo, kulikuwa na tamthilia nyingi zilizotungwa na kufikia kiwango cha kitaifa. Tamthilia zilizowasilishwa kwa wingi katika

maonyesho ya shule zilikuwa ni za Kiingereza, kwa mfano: *The Scourge* (1993), *The Stigma* (1994), *The Fruit* (1994), *The Spirogyra* (2001), *The Syndrome* (2001), *The Quarantine* (2005) na *The Umbilical Cord* (2005). Matokeo ya utafiti yalikusudiwa yawafaidi washika dau wote kama vile: walimu, wanafunzi, wasomi na wanavyuo katika idara za lugha, fasihi na isimu pamoja na wahudumu wa afya.

Utafiti huu ulijikita katika uchambuzi wa tamthilia na kuchanganua kipengele cha lugha. Mkurupuko wa magonjwa ya ukimwi na maafa yaliyotokea nchini, ni sababu zilizowashurutisha wasanii kutumia tamthilia ili kuelimisha umma dhidi ya ukimwi. Wasanii huwa ni walimu wa shule za msingi na upili, pamoja na wanavyuo, walio na ufundi wa taaluma ya tamthilia. Walimu huwashirikisha wanafunzi kwa kuwafunza mbinu za kimaigizo na kuwashirikisha katika mashindano ya kitaifa ya sanaa za maonyesho. Wizara ya Elimu nchini ndiyo hushughulikia maandalizi ya michezo ya kuigiza kwa madhumuni ya kuwaelimisha wanafunzi kwa kukuza vipawa vyao vya uigizaji na vilevile vya matumizi ya lugha. Mashindano haya yamesaidia Wizara ya Elimu kuwa kipaumbele kupambana na vita vya ukimwi. Wizara ya Elimu imeweza kuihamasisha umma kupitia sanaa ya nyimbo na michezo ya kuigiza yenye mada kuhusu janga la ukimwi. Taasisi ya Elimu (K.I.E) imekuwa ikikusanya kanda za video na kuzihifadhi ili zitumiwe katika nyanja za elimu na shuleni. Hata hivyo, ni kiasi kidogo tu cha hadhira ambacho kiliwahi kupata nafasi kumiliki au kutazama kanda hizo. Ingawa tamasha za sanaa za maonyesho hufanyika kila mwaka katika makumbi makuu ya kitaifa, ni wananchi wachache tu waliowahi kushiriki. Kwa hivyo, utafiti huu unalenga kutathmini vipengele vya lugha vipengele vya lugha lugha

vinavyotumiwa katika michezo ya kuigiza kuhusu ukimwi katika mashindano ya sanaa za shule za upili.

MAPITIO YA MAANDISHI

Kipengele cha lugha kilikuwa sehemu muhimu zaidi kwa kuwa kilitumiwa kupashia ujumbe. Mtunzi alitumia lugha kama malighafi muhimu ya kuijengea kazi yake. Mbali na kuelezea lugha kama mfumo wa ishara za sauti zilizopangwa kwa njia maalum. Aswani (2006) alielezea kuwa chombo hiki kilikuwa hakina uhusiano wa moja kwa moja kati ya sauti au hati zilizoandikwa, na kile kilichoashiriwa. Uhusiano uliopo ulikuwa ni wa kisadfa tu, isipokuwa kwa maneno ya miigo ya hali, vitu na wanyama. Lugha ya kisanaa ndiyo iliyotofautisha fasihi na sanaa zingine kama vile, uchongaji, uchoraji na ufinyanzi.

Njogu na Chimera (1999), walifafanua majukumu ya lugha ya kifasihi. Walieleza kuwa kile kinachotofautisha lugha ya kifasihi na lugha nyingine ni ule uwezo wa fasihi kuifanya lugha ya kawaida ionekane kana kwamba yavutwavutwa, yafinyangwa finyangwa na kupondwapondwa. Lugha ya fasihi ilionekana ngeni, na kwa sababu ya ugeni wake, ulimwengu wa kawaida ulikuwa mgeni, usiokuwa wa kawaida. Lugha ya kifasihi iligeuza lugha ya kawaida, ikakiuka kaida zake, kupitia matumizi ya nguvu dhidi ya lugha na kuifanya iwe teule. Lugha ya kifasihi ilikuwa na nguvu kutokana na uwezo wa kutumia mbinu za lugha ya kitamathali na ya kiishara.

Mwamzandi (1996), alihakiki utanzu wa ushairi na kutambua sifa bainifu zilizotofautisha lugha ya kawaida na ya kisanaa. Mwamzandi alihakiki nguzo

sita muhimu zilizoweza kutumiwa kufasiri maana katika muktadha. Lengo msingi katika utafiti wake ni uchambuzi wa maana kama kipengele cha mawasiliano. Mwamzandi alitumia nadharia ya semiotiki katika uhakiki wake. Tofauti ya utafiti wa Mwamzandi na huu, ni kuwa Mwamzandi alishughulikia kipengele cha maana katika sanaa ya ushairi. Utafiti huu mbali na kuchambua kipengele cha maana katika tamthilia, ulichanganua mbinu, maudhui na lugha ya kisanaa iliyoitumiwa na wasanii katika ujenzi wa tamthilia. Vilevile, tulichunguza maumbo mbalimbali yaliyojenga tamthilia.


Aristotle aliwalaumu watunzi wa mashairi kwa matumizi mengi ya kibalagha. Alidai kuwa fani hii ilidhoofisha uhalisia wa kifasihi. Aristotle alieleza kuwa watunzi wa mashairi waliwakuza wahusika wao zaidi ya sanaa yenyewe. Hakupendezwa na uhuru wa lugha ya ubunifu iliyoitumiwa na watunzi wa mashairi kwa kuwa ulikuwa na ukiukaji mwingi wa kaida za lugha. Washairi waliboronga miundo ya masimulizi, wakapunguza maumbo ya maneno na kupoteza ujumbe kwa kutumia lugha yenye maana fiche. Watunzi walifanya hivi kwa kuwa walikuwa wakishindana na kuonyesha ustadi wao wa utunzi. Alichukizwa pia na watunzi wa maigizo waliowakuza wahusika wao na kuwapa nguvu za kiungu zilizoambatana na ushirikina. Wahusika hawa walitatu matatizo yao kupitia nguvu zao za kimiujiza na mazingaombwe. Hii ilifanya wahusika kupoteza uhalisia wa kibinadamu. Dhana hii wa uumbaji wa wahusika ndiyo iliyozua kichocheo cha kwanza cha uhakiki kilichojulikana kama uhakiki wa Ki-aristotle.

Upatanifu na muumano wa sehemu mbalimbali za tamthilia kama vile: muundo, taashira, maudhui na

maana zilihusiana na kusaidiana. Ni kupitia lugha ndipo maudhui yaliweza kusafirishwa, dhamira kufikia hadhira na maana kusimbuliwa na hadhira. Matokeo yalionyesha kuwa lugha ya kifasihi ilikuwa maalumu na iliyotofautiana na lugha ya kawaida. Uteuzi wa maneno yaliyochaguliwa, ujenzi wa wahusika, ujenzi wa mandhari, matumizi ya mbinu za kifasihi kama vile

njozi, viona mbele, mbinu rejeshi, mchezo ndani ya michezo, zilikuwa ni ishara zilizoashiria ujumbe kupitia lugha na zilihitaaji hadhira kufasiri maana fiche iliyolengwa. Nguvu hii ya lugha ya uwasilishaji ndio iliyofanya kazi ya kifasihi iwe tofauti na kazi ya lugha zingine.

Mchoro wa: Misingi ya nadharia



Chanzo: Mtafiti (2009)

Misingi ya nadharia ya utafiti ilielezwa kupitia mchoro 1. Wazo tama lilionyesha kuwa kulikuwa na uhusiano kati ya lugha na ujumbe. Lugha ilikuwa kisababishi kilichofanya ujumbe ujitokeze vyema katika utunzi wa tamthilia. Kwa hivyo, ujumbe ulikuwa ni kibadiliki kilichotegemea lugha. Tamthilia ilitegemea lugha ya kisanaa kuijenga (sehemu B). Lugha ya kisanii iligawanywa katika sehemu mbili kuu zilizoongozwa na nadharia ya semiotiki na umuundo. Semiotiki ilizua lugha za kiishara (sehemu C), nao umuundo ulizua

maumbo ya uamilifu wa utendakazi wa kila kiambajengo kilichojenga tamthilia, (sehemu D). Sehemu ya taashira ilibainisha (sehemu E na F) ambazo ni vipengele vya maana na tamathali za semi. Sehemu ya muundo nayo ilibainisha vipengele viwili pia (sehemu G na H), ambazo zilijengwa kwa maumbo ya nje na ya ndani ya tamthilia. Sehemu hizi (E, F, G na H) zilikuwa muhimu kwa kuwa ndivyo vilikuwa vigezo vya kupimia nguvu ya uwasilishi wenye muwala wa kimantiki. Vijisehemu vyote vya tamthilia

vilitagemeana kupitia utaratibu maalum uliofuatwa. Sehemu hizi zote zilijumuika pamoja na kuzua ujumbe ulioeleweka moja kwa moja (sehemu I). Ili ujumbe upate kuwasilishwa, vizuri kulitegemea usukaji mzuri wa lugha ya kitaashira na muundo.

MATOKEO YA UTAFITI

Kipengele cha lugha ndicho kilichotumiwa kubainisha kazi ya fasihi na lugha ya kawaida. Lugha ndiyo iliyokuwa mzizi wa kazi yetu. Lugha ya maneno ndiyo iliyotumiwa kufafanua maudhui kwa njia ya kisanaa. Madhumuni ya utafiti wetu yalikuwa kutathmini vipengele vya lugha vilivyotumiwa kuzijenga tamthilia za shule. Matokeo ya uchanganuzi wa data yetu yalionyesha kuwa kipengele cha lugha kiligawanywa katika matanzu matatu makuu. (kama ilivyoelezewa katika mchoro 1, wa misingi ya nadharia). Nadharia ya semiotiki na umuundo zilitusaidia kuainisha lugha katika matapo matatu

Utanu wa kwanza ulichunguza lugha kupitia mbinu za lugha ambazo ziligawanywa katika mafungu ya umuundo na taashira. Vipengele vya umuundo navyo viligawanywa kupitia sehemu za muundo wa ndani na wa nje. Mafungu ya maumbo ya nje yalijumuisha anwani, onyesho na maonyesho na maelezo katika mabano. Maumbo ya ndani yalijumuisha umilisi wa wahusika, mandhari, jumuiya na kadhalika. Kipengele cha taashira kiligawanywa kupitia vipengele vya maana katika viwango vya isimu kama vile mofolojia, pragmatiki na fonolojia. Kipengele cha pili kilikuwa cha kitaashira na kilijumuisha tamathali za semi. Tamathali zilizotumiwa zilikuwa ni: jazanda, taharuki, tashbihi, tasfida, udamisi, tashisi. Utanu wa tatu ulifafanua matumizi ya lugha hasi au chanya. Lugha hasi ilitumiwa kukuza maudhui ya matukio hasi katika

jamii kama vile: unyanyapa, ukimwi, utasa, uana, uhafidhina, mila na utamaduni, taasubi za wanaumme na kadhalika.

Kupitia uchanganuzi wa data, tulitambua mahusiano kati ya lugha ya tamthilia na ujumbe. (Mchoro 1 ya misingi ya nadharia). Lugha ya sanaa ilikuwa kisababishi cha ujumbe. Wanamuundo walielezea kuwa kazi ya fasihi ilikuwa kongomano la mbinu mbalimbali za lugha zenye majukumu mbalimbali tofauti katika muundo mzima. Lugha ilikuwa ni nguzo kuu katika sehemu na kongomano zote katika kazi ya kifasihi na ilitumiwa kuwasilisha ujumbe wa ukimwi. Lugha pia ilitumiwa kufafanulia visehemu vyote vya tamthilia kama vile: maudhui, mbinu za sanaa na maana.

MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Tamathali za semi zilitumiwa katika tamthilia zote mbili. Hizi zilikuwa: jazanda, kinaya, methali, taharuki, kuchanganya ndimi, balagha, udamisi, uzungumzi nafsi, tashbihi, tashisi na kadhalika. Mbinu ambazo zilitumiwa kwa wingi katika tamthilia zote zilikuwa ni za methali, taharuki, monolojia, uzungumzi nafsi, semi na tasfida. Lugha ya kisaniai ilitumiwa katika tamthilia za shule za upili. Lugha iligawanywa kwa mifumo ya mbinu za kiishara na viambajengo vya umuundo. Mifumo ya ishara, maana ya lugha ya kiisimu na taashira za lugha zilitumiwa kujenga tamthilia.

Mapendekezo: Kupitia maelezo ya misingi ya nadharia (mchoro wa 1), yalibaini kuwa ili tamthilia ijengwe vizuri kwa njia ya kisanaa ilihitaji lugha yenye mvuto na mnato kusababisha ujumbe uliofaa. Kutokana na matokeo kulikuwa na mahusiano makubwa kati ya ujumbe na lugha, wasanii walihita

kufanya utafiti mkubwa zaidi kuhusu sanaa ya lugha kwa kuwa ndiyo sehemu ya umuundo ilihitaji ufundi mkubwa. Hata hivyo, kulikuwa na matumizi ya lugha ya ishara na umuundo katika ujenzi wa tamthilia hizi za shule za upili. Kwa kuwa hadhira kubwa ya

watazamaji na waigizaji ni wanafunzi wa shule za upili, kulihitajika kiwango cha lugha ambacho kingeliwaafiki na kilicho katika himaya yao ya matumizi.

REFERENCES.

- Aswani, B. (2006). *Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Jomo Kenyatta Foundation.
- Mwamzandi, I. (1996). *Mbinu za Kimaigizo katika Tungo za Abdilatiff Abdalla*. Chuo Kikuu Cha Egerton: Tasnifu ya M.A.
- Njogu, K., & Chimerah, R. (1997). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.